HABARI LEO UK 19

a kazi

funzi
ka chuo
nahiri
oma.
ake
raza la
Mjema
tekeleza
iane
ino
bayo
dana
deleo
Taifa
.
amoja
o ya
u,
zi,
a mi-
ion-
ya
ha
a

10

# Serikali yakataa kufungua kiwanda cha kuchinja punda

**Na Kareny Masasy, Shinyanga**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amekataa kukifungua kiwanda cha kuchinja punda cha Fang Hua kilichopo Kata ya Ibadakuli Manispaa ya Shinyanga kutokana na kushindwa kukidhi masharti waliyopewa na wizara kuwa na ranchi yenye punda wao, mkataba na wafugaji pamoja na mtambo wa kuchinjia wenye ubora.

Ndaki aliyasema hayo jana alipotembelea kiwandani hapo na kueleza mbele ya meneja wa kiwanda hicho, Jiao Zhiling kuwa ranchi inaonekana haina punda na wanaowamiliki wao ni punda 386 mpaka sasa na kila siku wanatakiwa kuchinja punda 20 kwa mujibu wa mkataba.

Alisema kuwa wawekezaji wa punda hapa nchini wanatakiwa kufuata masharti na kuwa kiwanda hicho kilisimamishwa tangu mwaka jana na kufunguliwa mwaka huu mwezi Aprili na kupewa muda wa miezi sita waboreshe, lakini walichoboresha ni chinjio pekee kwa sababu walikuwa wakiwapiga na nyundo punda kitendo ambacho ni kinyume na utaratibu.

"Tulivyositisha uzalishaji wa mazao ya nyama kiwandani hapo mwezi mmoja wakaandika barua wizarani kwa madai wamekwishaboresha na kifunguliwe... leo nimejionea mwenyewe kwa masharti wanatakiwa kuchinjwa punda 20 kwa siku na mpaka sasa kiwanda kina punda 386 si wataisha ndani ya mwezi mmoja, sababu ya kuwataka wawe na punda ni ili wafanye uhimilishaji na kuzaliana kwa wingi," alisema Ndaki.

Mkurugenzi wa huduma za mifugo nchini, Profesa Hezron Nonga alisema kuwa mwaka 2017 serikali ilisitisha kuchinjwa wa punda, kwa sababu waliona masharti ya uchinjaji yanakiukwa ya kuchinja punda kuanzia 150 hadi 200 kwa siku na baadaye ikarudisha kwa kutoa masharti ya kuchinja punda 20 kwa siku wanachokiuka hawa wamekuwa wakitumia mawakala wao vijijini kuchinja punda na kuleta nyama kiwandani kwa ajili ya kusafirisha.

"Sisi tumewabaini wanachinja punda kinyemela, tena uchinjaji wa haramu na hivi sasa kuna punda 500,000 nchi nzima, tunataka nao wafuge ili angalau wakifika punda milioni tatu itasaidia kwenye uzalishaji wao kiwandani... kinachofanyika ni uhuni hawana punda na wengine walikuwa wakitoroshwa na mawakala wao kwa njia za panya sasa wanataka kifunguliwe na maeneo waliyoelezwa bado hawajayaboresha," alisema.

Scanned with CamScanner

hayo, bodi ya kampuni hiyo kwenye kikao cha Ijumaa itatoa mapendekezo ya gawio kwa wanahisa wake na yakiridhiwa malipo hayo yatafanyika mwaka huu.

muda usiojulikana uzalishaji wa vinywaji katika kiwanda cha Tanbus kilichopo wilayani Rombo kwa madai ya vinywaji

kinywaji aina ya banana kuwa na viwango vikubwa vya kemikali ya aside ambayo haifai kwa matumizi ya binadamu.

kadhaa amefika kiwandani hapo na kuagiza kuchukuliwa kwa sampuli ya pombe hiyo na kubaini haikuwa

alipochukua sampuli nyingine alibaini kilevi cha asilimia 12, jambo ambalo siyo sahihi.

Happy Kanyika ... kufungwa kwa kiwanda hicho kutokana na kukosa ubora.

HABARI LEO UK 17

# *Bara, Visiwani waweka maazimio kuboresha sekta ya mifugo*

**Na Mwandishi Maalumu**

MAKATIBU wakuu wa sekta ya mifugo Tanzania Bara na Visiwani wamekutana na kuweka mikakati ya kuendeleza sekta hizo kwa ajili ya wafugaji wa pande mbili za Muungano ambapo maazimio saba yameridhiwa ikiwa ni hatua ya kufikia malengo tarajiwa.

Maazimio hayo yamefikiwa juzi wilayani Chake-chake, Pemba, kwenye kikao kilichowakutanisha Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (mifugo), Amosy Zephania na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kutoka Serikali ya Zanzibar, Maryam Juma Sadallah.

Zephania alisema kuwa kwa kuendelea kushirikiana kupitia vikao na utekelezaji wa maazimio yanayoridhiwa na pande zote mbili, sekta ya mifugo itapiga hatua na kunufaisha wananchi kiuchumi kulingana na idadi kubwa ya mifugo iliyopo nchini.

Alisisitiza kuwa ni vyema wataalamu wa sekta ya mifugo Tanzania Bara na Zanzibar wakaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi kiutendaji kwa ajili ya kubadilishana uzoefu ili kupunguza au kuondoa kabisa kero na changamoto zinazowakabili wafugaji.

Kwa upande wake, Maryam aliipongeza timu ya wataalamu wa sekta ya mifugo Tanzania kwa utekelezaji wa kiwango cha hali ya juu wa maazimio ya kikao kilichofanyika Juni 4, 2021 jijini Dar es Salaam.

Aliwataka wataalamu kushirikishana kwenye mipango kazi yao ili iwe rahisi kusaidiana pia kutumia fursa zinazopatikana kwa faida ya pande mbili za Muungano akitolea mfano wa baadhi ya miradi ya miundombinu ya mifugo inayotarajiwa kujengwa Zanzibar kwa mkopo wa dola za Marekani milioni 60 kutoka nchi ya Hungary.

Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba, Hakim Vuai Shein aliwapongeza wataalamu hao kwa utekelezaji wa maazimio mbalimbali na kusisitiza kuwa matarajio ya wadau wa sekta ni kuona changamoto zao zinafikia mwisho.

Baadhi ya maazimio yaliyofikiwa kwenye kikao hicho cha ushirikiano baina ya wizara hizo mbili ni pamoja na makubaliano maalumu kati ya Taasisi za Utafiti na Mafunzo.

Azimio lingine ni uzalishaji wa mifugo hususani mitamba ya ng'ombe chotara ambapo Tanzania Bara itatoa mbegu za mifugo dozi 1,000 kwa ajili ya kuwezesha uhimilishaji kwa wafugaji wa Zanzibar.

Lingine ni kufanya uchambuzi wa mnyororo wa gharama za uzalishaji wa mifugo na mazao yake na kuandaa maandiko ya miradi ya pamoja.

Scanned with CamScanner

UHURU UK 9.

# Sekta ya mifugo Bara, Z'bar waweka mikakati

**Na MWANDISHI WETU, Zanzibar**

MAKATIBU wakuu wa sekta ya mifugo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), wamekutana na kuweka mikakati ya kuendeleza sekta hizo kwa wafugaji wa pande zote.

Katika mkutano wao, makatibu wakuu hao wameridhia maazimio saba yakiwa hatua ya kufikia malengo tarajiwa.

Maazimio hayo yamefikiwa juzi, wilayani Chakechake Pemba, katika kikao kilichowakutanisha makatibu wakuu kutoka sekta ya mifugo ya SMT, Amosy Zephania na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo wa SMZ, Maryam Juma Sadallah.

Akifungua rasmi kikao hicho, Kaimu Katibu Mkuu Sekta ya Mifugo wa SMT, Amosy Zephania, aliishukuru sekta hiyo kwa upande wa SMZ kwa maandalizi mazuri ya kikao hicho ambacho kilitanguliwa na kikao cha siku moja cha wataalamu wa sekta hizo kutoka pande hizo.

"Vikao hivi tuvipe umuhimu wa kipekee ili tuweze kufanya tahmini ya maendeleo ya sekta zetu," alisisitiza.

Zephania aliongeza kuwa, kwa kuendelea kushirikiana kupitia vikao na utekelezaji wa maazimio yanayoridhiwa na pande zote, sekta za mifugo zitapiga hatua na kunufaisha wananchi kiuchumi kulingana na idadi kubwa ya mifugo iliyopo nchini.

Bw. Zephania alisisitiza kuwa ni vyema wataalam wa sekta za Mifugo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuendelea kushirikiana kwa karibu zaidi kiutendaji kwa ajili ya kubadilishana uzoefu ili kupunguza au kuondoa kabisa kero na changamoto zinazowakabili wafugaji wa Tanzania.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo wa SMZ, Maryam Juma Sadallah, alishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuendelea kushirikiana nao ikiwa pamoja na kutimiza makubaliano ya kukutana kupitia vikao kazi kama walivyokubaliana.

Maryam aliipongeza timu ya wataalamu wa sekta za mifugo kutoka pande mbili hizo kwa utekelezaji wa kiwango cha hali ya juu wa maazimio ya kikao kilichofanyika Juni 4, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

"Nawapongezeni wataalamu wetu kwa kazi nzuri mliyoifanya ingawa sio kwa asilimia 100, lakini mmejitahidi sana," alisema Maryam.

Aidha, aliwataka wataalamu kushirikishana katika mipango kazi yao, ili iwe rahisi kusaidiana, pia kutumia fursa zinazopatikana kwa faida ya pande mbili za muungano akitolea mfano wa baadhi ya miradi ya miundombinu ya mifugo inayotarajiwa kujengwa Zanzibar kwa mkopo wa dola za Marekani milioni 60 kutoka nchi ya Hungary.

Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba, Hakim Vuai Shein aliipongeza timu ya wataalamu kwa utekelezaji wa maazimio mbalimbali na kusisitiza kuwa, matarajio ya wadau wa sekta ni kuona changamoto zao zinafikia mwisho.

Scanned with CamScanner

uzalishaji wa bidhaa hizo, jambo ambalo linaipelekea serikali kuwa na imani.

Pia, aliwataka wamiliki wa kiwanda hicho kuwa wabunifu ili kuongeza kasi ya ushindani na kuongeza uzalishaji

Hemed.

Katika hatua nyingine, Makamu wa Pili wa Rais, alimuagiza Kamishna wa Kazi kuhakikisha anafuatilia malalamiko ya wafanyakazi wa kiwanda hicho na kuyapatia ufumbuzi

80 ya wafanyakazi katika kiwanda hicho ni Wazanzibari, jambo ambalo limesaidia kufikia shabaha ya serikali kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya kutoa ajira 300,000.

UHURU UK 10

WAFUGAJI

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na ujumbe wa wawekezaji wa Misri ukiongozwa na Kiongozi Mkuu ya Kampuni ya Elsewedy.Mhandisi Ahmed El Sewedy (wa pili kulia), baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Maonesho ya Wafanyabiashara wa Nchi za Afrika, jijini Durban, Afrika Kusini, juzi. Kushoto kwa Rais ni Waziri wa Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaban. (Picha na Ikulu).



# Wataalamu wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili watakiwa kushirikiana

WATAALAMU wa Sekta ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, wametakiwa kuongeza ushirikiano katika kujadili na kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Akizungumza jana katika kikao cha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Amosy Kulwa Zephania alisema, ushirikiano ni muhimu katika kulijenga na kuliendeleza taifa kiuchumi.

Katibu huyo alisema kilimo na mifugo ni msingi katika kuliendeleza taifa kiuchumi, hivyo ni wajibu wa wataalamu kutafuta namna bora itakayowasaidia wakulima na wafugaji kunufaika na shughuli hizo.

"Ni muhimu kukutana na wataalamu kujadili jambo hili, tunasaidia kuchangia maisha ya watu kutokana na kuwa kilimo na mifugo ndio uti wa mgongo wa wananchi wetu," alisema.

Alisema kuwepo vikao kutaziwezesha wizara hizo mbili kupata utaalamu mpya wa kuweza kuinua sekta ya kilimo kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar Maryam Abdalla Sadala alisema, mifugo na mazao yaliyopo yanawanufaisha wananchi wa Tanzania, hivyo wataendelea kushirikiana ili kuwa na uchumi jumishi kwa jamii yao.

"Ushirikiano huu tunaamini utazaa matunda tunakaa pamoja kubadilishana mawazo na kutafuta mbinu mbadala ya kuwasaidia wananchi wetu kutatua changamoto zinazowakabili ambazo tunazipendekeza kwenye vikao vyetu," alisema.

USHIRIKIANO

## CHANGAMOTO

Alisema kilimo na mifugo ni msingi katika kuliendeleza taifa kiuchumi, hivyo ni wajibu wa wataalamu kutafuta namna...

Scanned with CamScanner

buni Zanzibar.

Hemed alifurahishwa na hatua ya maendeleo ya kiwanda hicho katika uzalishaji wa bidhaa

ja kuona bi katika kiwan na zinauzika da wa Afrika bayo inaenda

MWASHE UK 17

# DC sasa aonyesha fursa kwa wavuvi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja, Suzan Peter Kunambi, amewataka wavuvi kujiunga katika vikundi ili kufanya kazi zao kwa ushirikiano na ni rahisi kupata fursa zinazotolewa na serikali ikiwamo mikopo.

Aliyasema hayo jana Mtoni Kigomeni alipokuwa akizungumza na wavuvi wa eneo hilo, kwa lengo la kuwahamasisha kuanzisha vikundi vya ushirika.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeandaa programu maalum ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na wavuvi ni moja kati ya kundi litakalonufaika na mpango huo hivyo ni vyema kuwa tayari kwa kufuata masharti na watakaonufaika na fursa hiyo ni wale watakaokuwa wamesajiliwa.

Alisema kuwa mikopo hiyo haitakuwa na riba wala masharti magumu bali itatolewa kupitia Shirika la Fedha Duniani (IMF) zilizotolewa kwa ajili ya kupambana na UVIKO-19.

Mkuu huyo wa Wilaya alizitaja fursa zinazotarajiwa kutolewa na serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Bluu ni kuwapatia wavuvi boti zenye mashine na zana zote za uvuvi na mafunzo maalum ya teknolojia bora ya uvuvi.

"Dhamira ya serikali ni kuleta mageuzi makubwa katika shughuli zote zinazofanywa na wavuvi wa maji madogo. Lakini katika eneo la bahari kuu ili kupata maendeleo ya haraka na kuimarisha uchumi wa bluu nchini," alisema.

Wakieleza changamoto zao, wavuvi hao, walisema miundombinu katika eneo hilo wanaliotumia kwa ajili ya shughuli za uvuvi hairidhishi pamoja na kukosekana kwa huduma ya majisafi na salama na huduma za vyoo katika eneo ni changamoto inayowasababishia usumbufu katika shughuli zao.

Scanned with CamScanner

franchise senior manager, Hellen Masumba. Photo: Guardian Correspondent

THE GUARDIAN Page 4

# Livestock minister declines to inaugurate donkey meat plant

**By Guardian Correspondent, Shinyanga**

LIVESTOCK and Fisheries minister,Masimba Ndaki declined to officially inaugurate the Fanghua donkey meat processing plant for export located at Ibadakuli in Shinyanga Municipality.

This was during his inspection visit at the factory to see whether the owners thereof had abided by the government conditions given last August.

Ndaki said since the conditions given had not been met, he couldn't to inaugurate the factory until such time the conditions are met.

"When we opened the factory's construction, the government gave a condition to owners to establish a donkey ranch, provide donkey keepers production contracts and to import the animals from China for cross breeding, and that they should never buy them from the people, the practice that would endanger their populations," said the Minister.

He added: "Since there hasn't been any implementation of the conditions, I will not inaugurate the factory until such time the conditions are met."

He also called on local investors to abide by the country's laws and other procedures, it should not be seen that they are being subjected to some humiliation from the government, adding "the government does not want to eradicate the

For his part, the donkey plant manager Jiaozhili Ing said they have done many renovations to the factory and that is why they called in the government to inaugurate it.

He said as for now they have already established a 33-acre donkey ranch in Kishapu District and have started keeping for donkey production and so far there is a total of 20 animals, and promised to deal with the other conditions given.

banana liquor is not fit for human consumption," he said.

down all liquor factories in Rombo District," he said.

THE GUARDIAN Page 4

# Union, Z'bar livestock sectors chart development strategies

**By Guardian Correspondent, Pemba**

LIVESTOCK sectors of the Union and Zanzibar Governments, through their Permanent Secretaries have met to chart strategies to develop the sectors for livestock keepers of both sides and seven resolutions have been endorsed.

The resolutions were reached on Monday this week in Chakechake District, Pemba at a meeting that brought together Permanent Secretaries - Amosy Zephania, Acting Permanent Secretary from Tanzania Ministry of Livestock and fisheries and his Zanzibar counterpart, Ms Maryam Juma Sadallah.

Officially opening the meeting, Amosy Zephania thanked the Zanzibar Livestock sector for the good preparation of the meeting that was preceded by a one-day meeting of the sectors' experts.

Zephania further said by continuing collaboration through meetings and the implementation of the endorsed resolutions, the livestock sectors will make great strides to economically benefit the people of both sides of the Union.

He stressed that it would be better for experts from the livestock sectors of the two governments to continue working together closely through exchange of experience and reducing, or completely eliminating all challenges facing Tanzania livestock keepers.

For her part, Zanzibar ministry of Livestock and Fisheries permanent secretary, Maryam Juma Sadallah, welcoming her Mainland counterpart, thanked Tanzania's Ministry of Livestock and Fisheries by continuing collaborating with them including further meetings as had been agreed.

She also praised the team of livestock sectors experts from both sides of the Union for implementing the resolutions of the sitting of June 4 2021 at TVA hall in Dar es Salaam.

She also called on the experts to work together in their work plans so it becomes easy to assist each other, and cited the example of the infrastructure construction projects earmarked for Zanzibar from USD 60 million funding by Hungary.

For his part, Hakim Vuai Shein, the Sponsoring Officer from the Ministry of Agriculture, Irrigation, Natural resources and Livestock from Pemba praised the team of experts for implementing various solutions, saying it was the expectation of many that challenges facing the sectors are addressed.

Among the resolutions include the existence of special agreement in research and training intuitions, production of livestock especially hybrid cows whereby the Zanzibar government will provide 1,000 doses for Zanzibar livestock keepers, and assessing the value chain on livestock and their products.

Scanned with CamScanner